



TANGAZO

UUZAJI WA MITI YA TEAK (MISAJI) KWA NJIA YA MNADA

KATIKA MASHAMBA YA MITI MTIBWA (MOROGORO) NA LONGUZA (TANGA)

1. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) unatarajia kuuza miti aina ya Misaji yenye jumla ya meta za ujazo **7,067.338** zilizopo katika shamba la miti Mtibwa Mkoani Morogoro na Longuza Mkoani Tanga. Jumla ya meta za ujazo **2,111.516** zinatarajiwa kuuzwa katika shamba la miti Mtibwa na meta za ujazo **4,955.822** katika shamba la miti Longuza. Mauzo haya yatafanyika **Mei 10, 2017** katika ofisi za shamba la miti Mtibwa saa nne na nusu (4:30) asubuhi na **Mei 12, 2017** katika ofisi za shamba la miti Longuza saanne na nusu (4:30) asubuhi. Uuzaji huu utafanyika kwa njia ya Mnada (Auction) kwa kuzingatia kanuni 31 (ii) ya Kanuni za Sheria ya Misitu za Mwaka 2004. Miti hii ya Misaji itauzwa mahali ilipo na jinsi ilivyo na mnunuzi hatakuwa na haki ya kudai fidia baada ya mauzo.
2. Kampuni au mtu binafsi anayetaka kushiriki mauzo kwa njia ya mnada anatakiwa kuwasilisha maombi kwenye bahasha iliyofungwa kuonesha nia ya kushiriki mauzo kwa njia ya mnada akiambatisha, Usajili wa kiwanda cha kupasua magogo (Mwaka 2016/17) na cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Aidha, anatakiwa aoneshe namba ya kitalu/vitalu, bei na ujazo anaotarajia kununua kama ilivyo kwenye jedwali namba 1 na 2 hapo chini.
3. Mnada utaendeshwa hadharani wakiwepo wanunuzi wote katika ofisi za Mameneja wa mashamba siku ya Jumatano **Tarehe 10 Mei, 2017** kwa shamba la Mtibwa na **Ijumaa ya tarehe 12 Mei, 2017** kwa shamba la Longuza. Mnada utaendeshwa kwa kufuata Sheria ya Misitu Sura 323.
4. Kila kiunga kitanadiwa peke yake kulingana na bei ya Ujazo iliyopo. Hata hivyo, bei ya juu iliyotolewa na mnunuzi wakati wa kufungua bahasha haitauzia wanunuzi wengine kuongeza bei zaidi ya iliyotajwa awali.
5. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania unawaalika wanunuzi kutuma maombi yao kwa ajili ya kufanya mnada katika Mashamba ya miti Mtibwa na Longuza ambapo mnunuzi anaweza kuchagua mojawapo kati ya vitalu vifuatavyo;

JEDWALI Na. 1: KIUNGA NAMBA MT 11 SHAMBA LA MITI MTIBWA

Na.	Jina la kitalu	Ujazo wa kitalu (m3)	Bei ya awali/kitalu/m3
1	MT 11- C8	400.05	700,000
2	MT 11- D4	300.51	700,000
3	MT 11- D5	203.48	700,000
4	MT 11- D6	203.87	700,000
5	MT 11- D7	301.20	700,000
6	MT11-T3	301.06	700,000
7	MT11-T4	200.05	700,000
8	MT11-T5	201.27	700,000
Jumla ya Ujazo		2,111.516	

JEDWALI Na. 2: KIUNGA NAMBA KH2B NA KH2C SHAMBA LA MITI LONGUZA

Na.	Jina la Kitalu	Ujazo kwa kitalu (m3)	Bei ya awali/kitalu/m3
1	KH 2B-PA04	403.62	750,000
2	KH 2B-PA06	401.40	750,000
3	KH 2B-PA08	452.35	750,000
4	KH 2B-KW 1	741.71	750,000
5	KH 2B-KW 3	303.59	800,000
6	KH 2C-01	549.72	800,000
7	KH 2C-02	663.41	800,000
8	KH 2C-03	597.02	800,000
9	KH 2C-04	641.21	800,000
10	KH 2C-05	201.75	800,000
Jumla ya ujazo		4,955.822	

Angalizo: Kila kiunga kitauzwa peke yake

8. Wakala wa Huduma za Mimitu Tanzania utatoa hati ya ushindi kwa mnunuzi aliyetaja kiwango cha juu kwa kila kiunga wakati wa mnada.
9. Mnunuzi atakayefanikiwa kununua miti ya misaji hataruhusiwa kusafiirisha magogo nje ya nchi kwa mujibu wa kanuni ya 50(1) ya mwaka 2004. Kusafiirisha Mazao ya Mimitu nje ya nchi ni baada ya kuyachakata kwa Mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 69 la mwaka 2006.

6. Makampuni na watu binafsi wanakaribishwa kutembelea viunga shambani wakati wa saa za kazi kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9:00) alasiri isipokuwa siku za sikukuu. Mameneja wa mashamba au wasaidizi wake watakuwepo kwa ajili ya maelekezo zaidi
7. Wanunuzi wanapaswa kuchukua na kusoma masharti ya uvunaji. Masharti hayo yanapatikana kwa Mameneja wa mashamba husika.
8. Bei ya kianzio kwa kila plot (kiunga) imeoneshwa katika Jedwali namba 1 na 2 hapo juu ikijumuisha 'VAT', 'CESS', 'LMDA', TaFF na FOREST ROYALTY.
9. Mnunuzi atakayeshinda atalipa asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani yote ya ununuzi siku tatu (3) baada ya mnada kufanyika. Fedha hizo hazitarudishwa. Asilimia sabini na tano (75%) iliyobaki italipwa ndani ya siku kumi na nne (14) baada ya mnada. Malipo yatafanyika katika akaunti ya mashamba ya miti Mtibwa na Longuza kama inavoonekana hapa chini;

i. SHAMBA LA MITI MTIBWA

AKAUNT Na. 22010000567

NMB – TULIANI.

ii SHAMBA LA MITI LONGUZA

AKAUNTI Na. 41901000015

NMB – MUHEZA.

10. Mnunuzi atapaswa kuwasilisha hati ya malipo (pay – in – slip) ya benki kwa meneja wa shamba husika kama uthibitisho wa malipo si zaidi ya siku tatu (3) baada ya malipo kufanyika.
11. Wanunuzi watakaoshinda watatakiwa kuondoa mazao yao katika kipindi cha mwezi mmoja baada ya kumaliza malipo yote.
12. Maombi yote yawasilishwe siku ya mauzo kabla ya saa 4:00 asubuhi. wanunuzi watakochelewa kuwasilisha maombi yao kwa siku na muda uliopangwa hawataruhusiwa kushiriki katika mnada.

limetolewa na

KAIMU MTENDAJI MKUU

S. L. P 40832

DAR ES SALAAM.